OFISI YA RAISI TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI
SHULE YA SEKONDARI MWANZI

E-MAIL:Mwanzisec@gmail.com
Phone: HEADMASTER 0757 104 653

S.L.P 37
MANYONI -SINGIDA

29.03.2022

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi____________________________
S.L.P __________

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI MKOA WA SINGIDA 2021.

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2021 Tahasusi ya HGL shule ya Sekondari Mwanzi iko umbali wa Kilomita moja na nusu (1.5) kaskazini mashariki mwa Halmashauri ya wilaya ya Manyoni.
Muhula wa masomo unaanza tarehe **25.07.2021**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kabla ya tarehe 26.07.2022 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 19.07.2022.

**2.0 Mambo ya kuzingatia**

**2.1 Sare za shule**

I. Suruali mbili (2) za dark blue zenye celebration 2 kila upande zisizobana kwa wavulana.
II. Sketi mbili (2) za dark blue zenye mshono wa V mbele, ndefu na zisizobana.
III. Shati nyeupe za mikono mirefu.
IV. Hijab za rangi nyeupe za cotton zisizo na urembo wowote (kwa waislamu wanaovaa)
V. Sweta za kijivu zenye shingo ya V. (zinapatikana shuleni)
VI. Tai za special za blue na strips nyeupe (zinapatikana shuleni)
VII. Viatu vyeusi vya kamba na visigino vifupi.
VIII. Soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana.
IX. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe kwa wasichana.
X. Mkanda wa ngozi mweusi kwa wavulana.

**2.2 Nguo za kushindia (shamba dress)**

I. Wavulana suruali mbili (2) nyeusi za kitambaa zenye celebration mbili (2) kila upande zisizobana.
II. Wasichana magauni mawili (2) marefu rangi ya pink ya kitambaa cha cotton, mshono wa solo na mikono ya shati.
III. T-shirt mbili (2) zenye nembo ya shule. (zinapatikana shuleni@12,000/=)
IV. Track suit nyekundu zenye stripes nyeupe kwa ajili ya michezo. (kwa wote)

**ANGALIZO.**
Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine zozote ispokuwa Kanga kwa wasichana, Taulo, na nguo ya kulalia na nguo za ndani. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzu atakayekaidi.

**2.3 Ada na Michango ya Shule**

a. Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh. 70,000/= unaweza kulipa kiasi cha Tsh. 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Ada hiyo ilipwe kwenye account ya shule Na. **50701100048** katika benki ya NMB (TAFADHALI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE PAYING SLIP)

b. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:

I. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati
II. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
III. Shilingi 20,000/ kwa ajili ya taaluma
IV. Shilingi 35,000/= kwa ajili ya wafanyakazi wasio walimu
V. Shilingi 2,000/= kwa kila nguo inayopigwa nembo ya shule.
VI. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza 5,000/= na 5,000/= kwa ajili ya bima ya afya CHF (wanafunzi wenye bima zao watatumia bima zao)
VII. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima
VIII. Shilingi 5,000/ fedha ya tahadhari

c. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:**

i. Ream ya karatasi A4 moja - aje nayo
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iii. Godoro la futi 2 ½
iv. Mashuka mawili (2 ) ya cotton ya pink kwa wasichana
v. Mashuka mawili (2 ) ya cotton ya light blue kwa wavulana
vi. Blanketi 1
vii. Chandarua 1
viii. Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli, kijiko na kikombe )
ix. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko
x. Dawa ya chooni Lita 5 kwa mwaka
xi. **Wasichana waje na Reki, Panga,** fagio la brashi laini (Soft broom) na fagio la chelewa
xii. **Wavulana waje na jembe na mpini wake, kwanja ,** fagio la brashi gumu ( Hard broom) na fagio la chelewa
xiii. Sanduku la bati
ix. Box File la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi
x. Madaftari makubwa (Counter book ) 7 au zaidi, mkebe, kalamu za wino, za risasi na rula.

## 3:0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii. Kugombana na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake/walimu /walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi /kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati / uhusiano wa jinsia moja / kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito / Kutoa mimba
xi. Kushiriki vitendo vya uhalifu/Siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii. Kusababisha au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
**xiv. Kumiliki/kukutwa/kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**
xv. Kudharau bendera ya Taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**AIDHA**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

( a ) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

( b ) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

( c ) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

( d ) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

( e ) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

( f ) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

( g ) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

( h ) Kutunza mali za Umma

**N:B** **Wanafunzi hawaruhusiwi :**

i. **Kuja na simu ( Simu zitakazotumika kwa mawasiliano kati ya mzazi na mwanafunzi ni za Patron na Matron tu, na Mkuu wa shule kama italazimu)**
ii. **Kuja na pasi ya umeme, redio au kifaa chochote cha umeme,**
iii. **Kusuka, kunyoa mitindo wala kufuga ndevu**

4.0 Mambo mengine yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi.

v. Medical examination form ambayo itajazwa na MGANGA MKUU wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

vi. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo yatakayotolewa na shule.

vii. **Nakala ya cheti cha kuzaliwa**

viii. **ORIGINA RESULT SLIP YA KIDATO CHA IV**

**ELIMU NI MAISHA**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWANZI**

………………………………

**BENAS D. MAGAFU**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MWANZI
S. L. P. 37
MANYONI

**HALMASHURI YA WILAYA YA MANYONI**
**SHULE YA SEKONDARI MWANZI**

## FOMU YA MAKUBALIANO

Mimi ………………………………………………………………………………………………

Naikubali nafasi hii ya kidato cha kwanza niliyopewa katika shule hii, na nakubali kutii sharia zote za shule zilizopo na zile zote zitakazotolewa kwa muda wowote. Aidha ninaahidi kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi watakao chaguliwa kwa mujibu wa sheria.

Ninaahidi kuwa mwaminifu na kuwa nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu wote kwa manufaa yangu na taifa lote kwa ujumla.

SAINI YA MWANAFUNZI ………………………………
JINA LA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………………
SAINI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………………
TAREHE ………………………………

JINA LA AFISA MTENDAJI WA KATA/KITONGOJI/MTAA ………………………………………………
SAINI ………………………………………………
TAREHE ………………………………………………

MUHURI WA OFISI ………………………………

**FOMU HII NA FOMU YA MEDICAL EXAMINATION ZIRUDISHWE SHULENI ZIKIWA ZIMEJAZWA KIKAMILIFU**

# MANYONI DISTRICT COUNCIL

**MWANZI SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 37**
**MANYONI**
**DATE: ……………………………**

To the medical officer

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

Dear Sir/Madam

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine MR. /Miss …………………………………………………………………………… as to his/her fitness as a full time student of MWANZI SECONDARY SCHOOL, may I kindly ask you to fill in the particulars in the form hereunder.

Yours Sincerely

………………………

**BENAS D. MAGAFU**

**HEADMASTER**

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER**

1. Blood count (white Blood cells) ……………………………………………………
2. Stool examination ……………………………………………………
3. Urine examination ……………………………………………………
4. Gestation (for girls only) ……………………………………………………
5. Veneral disease ……………………………………………………
6. TB test ……………………………………………………
7. E.N.T Problems ……………………………………………………
8. Defects of a) The left and right eye ……………………………………………………
   b) The chest ……………………………………………………
9. Any CHRONIC or FAMILY disease e.g. Epilepsy, Sickle cell etc. ……………………………………………………

**DECLARATION**

I have examined MR/MISS ………………………………………………………… and certify that he/she is physically fit/unfit to pursue his/her studies as stated above.

……………………………………………

**Signature of Medical officer**

……………………………………………

**Name of Medical officer**

**Designation** ……………………………………………… **Official stamp** ……………………………………………………